

HALMASHAURI YA MANISPAA TEMEKE

[Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Temeke]

Simu: +255 22-2928132/2928138/2928139

Fax: +255 22-292 8137

Baruapepe: temeke@temekemc.go.tz

Tovuti: <http://www.temekemc.go.tz>



OfisiyaMkurugenzi

92 Barabara ya Mandela/ Taifa

S.L.P. 46343,

15883 TEMEKE

DAR ES SALAAM.

Tarehe: 28/10/2021

TAARIFA KWA UMMA

MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA KUPITIA MPANGO WA MAENDELEO YA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO - 19

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imepokea jumla ya **Tshs 3,440,000,000** kutoka kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuboresha Miundombinu ya Elimu (Sekta ya Elimu Sekondari) na Sekta ya Afya. Fedha hizi zimeelekezwa kwenye maeneo ya vipaumbele vinavyogusa wananchi moja kwa moja kwa ajili ya kuwaondolea kero katika kuzifikia na kuzipata huduma za Afya na Elimu katika Manispaa ya Temeke.

Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kama zilivyo Halmashauri nyingine Tanzania itapokea fedha kwaajili ya kuboresha miundombinu na mazingira ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara wadogo.

2. Miradi itakayotekelezwa kutokana na fedha za Mpango wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19

NA	MRADI	IDADI	KIASI CHA FEDHA
1	Ujenzi wa vyumba vya madarasa ya shule za sekondari	157	3,140,000,000.00
2	Ujenzi wa jengo la huduma ya Dharura(EMD)	1	300,000,000.00
	JUMLA KUU		3,440,000,000.00

3. Mgao wa magari (sekta ya Afya)

Pia Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kama zilivyo Halmashauri nyingine Tanzania itapokea mgao wa magari katika sekta ya Afya

- Mgao wa gari la usimamizi wa huduma za Afya
- Mgao wa gari la wagonjwa (Ambulance)


Elihuruma Mabelya
MKURUGENZI
MANISPAA YA TEMEKE